

Innovations – New Ideas

Mapambano compost – Mboji aina ya mapambano

- Hutokana na rasilimali zinazopatikana kwa Ukaribu/ Mazingira yanayotuzunguka.

1. MADHUMUNI YA MBINU HII MPYA:

- kuboresha/ kuimarisha rutuba katika udongo/ hadhi ya udongo
- inasaidia udongo kuwa na uwezo wa kuhifadhi maji
- inasaidia kuboresha umbile la asili ya udongo/ Lainisha
- inaongeza mbolea kwenye Udongo

2. NAMNA YA KUTENGENEZA MBOJI YA MAPAMBANO:

- ili kutengeneza Mboji ya Mapambano hatua zifuatazo inabidi zichukuliwe:
 - i. Chimba shimo la mviringo au pembe mraba lenye vipimo vifuatavyo (mzunguko/ kipenyo 2.5m, kina 3.0m iwapo eneo unalochimba lina ugumu – 1.0m kipenyo na 1.0m kina cha shimo
 - ii. Weka ndani ya shimo majivu ya kuni kiasi cha 1 inchi kisha paka majivu kuta za pembeni kufikia urefu wa $\frac{1}{2}$ m
 - iii. Baada ya majivu weka nyasi laini za majani ujazo wa nusu futi ($\frac{1}{2}$ f)
 - iv. Baada ya hapo weka aina zozote za mata maluku zinazoweza kupatikana mpaka shimo lijae kidogokidogo kufikia ujazo wa $\frac{1}{2}$ m juu ya shimo
Mata maluku/ taka taka hizi zinajumuisha – samadi ya mifugo, matandazo ya mifugo, kinyesi cha kuku, majani yaliyofyekwa kando kando ya barabara na kwenye viwanja vya mpira, majani ya miti, mabaki ya chakula cha mifugo (majani na vyakula vilioyosindikwa, mabaki ya migomba , na mazao, majani ya katani, mabaki ya chakula, maji machafu yaliyoogea au kufulia kila siku na mikojo ya mifugo. Michanganyiko hii hupangwa moja baada ya nyingine
 - v. Baada ya shimo kujaa funika kwa nyasilaini endelea kumwagia maji debe 2 yaliyotumika kila siku, inakuwa kama shimo ambalo taka hutupwa
 - vi. Mara mvuke unapokoma kutoka kwa kawaida ni baada ya wiki $3\frac{1}{2}$ hadi 4, mbolea/ mata makuku hii huonekana kama udongo laini mchanganyiko wa rangi ya kikahawia na majivu huwa haina harufu wala athari inapoguswa kwa mikono mitupu
 - vii. Wakati wa kupanda nafaka tumia $\frac{1}{4}$ liter hadi $\frac{1}{2}$ liter ya mbolea katika shimo moja, haina madhara inapogusana na mbegu

Baada ya kupakua mboji peleka shambani tayari kwa kupandia. Baada ya kupanda mazao shughuli nyingine za kilimo kuendelea kama kawaida. Kama mbolea hii itatumika mwaka huu hurudiwa tena baada ya miaka 3.

Kwa kawaida huifadhiwa nje ya shimo kwa kufunikwa na nyasi laini.

3. USIMAMIZI NA UJENGENAZAJI:


- shimo la mboji lichimbwe sehemu ambayo hairuhusu maji ya mvua kutiririka ndani ya shimo. Kama ni sehemu yenye mwinamo, pajengwe kinga kuzunguka shimo. Kwenye kipindi cha kiangazi iwapo patatokea mchuruziko wa maji kwenje shimo yaimarishwe/ yasaidiwe ili kuboresha ufanisi. Wakati wa kujaza shimo, inabidi kuepuka vifaa aina ya plastiki na vyuma kwakuwa haviozi. Baada ya shimo kujaa lisifunikwe kwa udongo bali kwa nyasi laini ili kuruhusu mzunguko wa hewa wa mchanganyiko huo. Wakati wa kujaza mata muluku na mchanganyiko mingine endelea kujaza hadi juu ya shimo urefu $\frac{1}{2}$ mita ndipo ufunike kwa nyasi laini.

4. MANUFAA YA MBOJI YA MAPAMBANO:

- Manufaa yatanayoyana na matumizi ya mboji hii ni haya yafutayo katika shamba la mama SUZANE
 - Mavuno huongezeka kutoka gunia 3 kwa eka hadi gunia 20 kwa eka, kipato katika haya huongezeka
 - kupeleka watoto kwenye taasisi za elimu ya juu na kazi vyengenezo kwenye mashirika ya kimataifa
 - mama huyu ni mjumbe kwenye kamati utendaji kikanda kaiika shughuli za kilimo
 - anatambuliwa kama mkulima mvumbuzi
 - hapo awali alionekana kichaa lakini kwa sasa ni rasimali/ nyenzo.

5. EPUKA MAMBO YAFUATAYO:

- Ndani ya shimo pasiwekwe vijiti, matawi ya miti, plastiki na vifaa vya chuma kwa kuwa haviozi na vinaweza kuzuia taka vyingine kuoza.
- Vipimo vya shimo la mboji na mpangilio uwekaji michanganyiko



Katika shimo usiweke vipande vya nyuma au plastiki kwani haviozi kwa urahisi au visioze kabisa. Epuka maji ya zaida kwenye shimo hasa wakati wa majira ya mvua. Weka kinga kuzuia maji yasiingie kwenye shimo.

MAONI KUHUSU MBOJI YA MAPAMBANO

Matumizi ya mbolea hii yanaweza kuleta mabadiliko katika maeneo kame hapa Tanzania.

Technologia hii ni rafiki kwa mazingira na haina athari yoyote.

Iwapo mbolea hii itatumika itapunguza gharama zisizo za lazima za kununua mbolea za viwandani.

Wakulima 100 kutoka mkoani Dodoma wamepokea utaalamu wa mboji ya mapambano na wameanza kupata faida yake kuwani inalipa.